# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)2130852
Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz


*Unapojibu tafadhali taja:* **YALIYOJITOKEZA**
Kumb Na: NBS/S.40/21/469 Tarehe: 15 Oktoba, 2012

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI SEPTEMBA, 2012

### Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Desemba 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEPUNGUA HADI ASILIMIA 13.5

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Septemba, 2012 (Septemba, 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Sep-2011 | Ago-2012 | Sep-2012 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 122.53 | 140.79 | 141.67 | 0.6 | 15.6 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 105.66 | 126.49 | 127.11 | 0.5 | 20.3 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 109.56 | 123.44 | 124.22 | 0.6 | 13.4 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 121.69 | 135.71 | 141.71 | 4.4 | 16.5 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 114.23 | 123.01 | 123.74 | 0.6 | 8.3 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 102.29 | 105.31 | 105.35 | 0.0 | 3.0 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 110.78 | 114.20 | 116.12 | 1.7 | 4.8 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 98.23 | 96.58 | 96.58 | 0.0 | -1.7 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 101.08 | 112.16 | 112.50 | 0.3 | 11.3 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 105.79 | 110.75 | 110.75 | 0.0 | 4.7 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 111.53 | 127.53 | 131.00 | 2.7 | 17.5 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 106.47 | 115.89 | 115.33 | -0.5 | 8.3 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100.0** | **116.80** | **131.09** | **132.58** | **1.1** | **13.5** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 121.32 | 139.33 | 140.51 | 0.8 | 15.8 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 133.06 | 150.36 | 158.90 | 5.7 | 19.4 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 111.45 | 121.33 | 123.19 | 1.5 | 10.5 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 108.20 | 116.96 | 117.83 | 0.7 | 8.9 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Septemba, 2012 umeendelea kumepungua hadi kufikia asilimia 13.5 kutoka asilimia 14.9 mwezi Agosti, 2012. Kupungua kwa Mfumuko wa Bei wa mwezi Septemba, 2012 kunamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwezi Septemba, 2012 imeendelea kupungua ikilinganishwa na kasi ya kupanda kwa bei kwa mwezi Agosti, 2012. Hata hivyo, kwa ujumla Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 132.58 mwezi wa Septemba, 2012 kutoka 116.80 mwezi wa Septemba, 2011. Mfumuko wa Bei wa Vyakula na Vinywaji Baridi umepungua hadi kufikia asilimia 15.6 mwezi wa Septemba, 2012 kutoka asilimia 18.8 kwa mwezi wa Agosti, 2012.

### Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Badiliko la Fahirisi ya Bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limepungua hadi asilimia 15.8 mwezi wa Septemba, 2012 ikilinganishwa na asilimia 18.5 mwezi wa Agosti, 2012. Kwa upande mwingine, kasi ya ongezeko la bei kwa bidhaa zisizo za vyakula imeongezeka kidogo hadi asilimia 10.5 kwa mwezi wa Septemba, 2012 ikilinganishwa na asilimia 10.3 kwa mwezi wa Agosti, 2012.

### Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa majumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Septemba, 2012 umepungua hadi asilimia 8.9 ikilinganishwa na asilimia 9.2 mwezi Agosti, 2012. Kwa upande mwingine, Mfumuko wa Bei wa Nishati kwa mwezi Septemba, 2012 umeongezeka hadi kufikia asilimia 19.4 ikilinganishwa na asilimia 16.9 mwezi wa Agosti, 2012. Kuongezeka kwa Mfumuko wa Bei wa Nishati kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei za petroli kwa asilimia 11.4 na diseli kwa asilimia 6.8 kutoka mwezi Agosti, 2012 hadi mwezi Septemba, 2012

**Kielelezo Namba 1: Mwelekeo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Septemba, 2011 Hadi Septemba, 2012. (Septemba 2010 = 100)**




Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonyesha kuwa, katika kipindi kati ya mwezi Septemba, 2011 hadi Septemba, 2012, kumekuwa na mwenendo wa kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali kama inavyoonyeshwa na Fahirisi za bei. Mfumuko wa Bei umekuwa na mwenendo wa kupanda kutoka asilimia 16.8 mwezi Septemba, 2011 hadi kufikia asilimia 19.8 mwezi Desemba, 2011. Kuanzia mwezi Januari, 2012 mwenendo wa Mfumuko wa Bei ulianza kushuka kutoka asilimia 19.7 mwezi Januari 2012 hadi kufikia asilimia 13.5 mwezi Septemba, 2012.

### MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 1.1

Mfumuko wa Bei wa mwezi Septemba, 2012 umeongezeka kwa asilimia 1.1 ikilinganishwa na asilimia 0.7 kwa mwezi Agosti, 2012. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 132.58 mwezi Septemba, 2012 kutoka 131.09 mwezi Agosti, 2012. Kuongezeka kwa Mfumuko wa Bei kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei za bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa Mfumuko wa Bei ni pamoja na; mafuta ya taa kwa asilimia 2.4, mkaa kwa asilimia 8.0, diseli kwa asilimia 6.8, petroli kwa asilimia 11.4, bili za maji kwa asilimia 7.6, betri za gari kwa asilimia 1.4, vinywaji vikali (spirits) kwa asilimia 3.0, vyerehani kwa asilimia

1.1, jiko la gesi kwa asilimia 1.6, mabegi ya mikononi kwa asilimia 1.5 na ghrama za saluni kwa wanawake kwa asilimia 3.1. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia pia kuongezeka kwa Mfumuko wa Bei ni pamoja na; mahindi kwa asilimia 2.1, unga wa ngano kwa asilimia 1.0, unga wa muhongo kwa asilimia 3.5, ulezi kwa asilimia 7.0, nyama ya ng'ombe kwa asilimia 2.8, samaki wabichi kwa asilimia 6.8%, matunda kwa asilimia 5.9% and vyakula vilivyoliwa migahawani kwa asilimia 2.7.


### Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Septemba, 2010 Ikilinganishwa na Mwezi Septemba, 2012

Tafsiri: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inapima badiliko la uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania itaweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Fahirisi za Bei za Taifa unaongezeka, thamani ya fedha hupungua.

Thamani ya shilingi 100 imeendelea kupungua hadi Shilingi 75 na senti 43 kutoka mwezi Septemba, 2010 hadi Septemba 2012

## MIENENDO YA BEI

### Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei Kutoka Septemba, 2011 Hadi Septemba, 2012. (Septemba 2010 = 100)




Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonyesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei kuanzia mwezi Septemba, 2011 hadi mwezi Septemba, 2012. Kwa wastani, Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi na Fahirisi za nishati na mafuta zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi zingine. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo za chakula pamoja na nishati zimeonyesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**